



WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUMU  
TAASISI YA MAENDELEO YA JAMII TENGERU



**TANGAZO LA ZABUNI YA UPANGISHAJI WA MAJENGO/ VYUMBA VYA**

**BIASHARA**

**TAREHE: 10/6/2022**

1. Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru anawatangazia makampuni ,watu binafsi, vikundi na taasisi zilizosajilwa na kuendeshwa kwa mujibu wa sheria , kanuni na taratibu za nchi nafasi za kupanga vyumba katika majengo ya taasisi kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kwa mwaka 2022/2023.
2. Tangazo hili linatolewa kwa wananchi wote kwa muda wa siku saba(7) kuanzia tarehe 10/6/2022 hadi tarehe 17/6/2022 kuweza kutuma maombi.
3. Zabuni hizi zinatangazwa kwa makampuni,watu binafsi, vikundi na taasisi zenye sifa ,weledi na uwezo wa kupangisha na kutoa huduma zifuatazo;-

NA	ZABUNI	NAMBA YA ZABUNI	JENGO
1	Ukodishaji wa cafteria	PA/128/2022/2023/H Q/NC/09	STUDENT CAFTERIA
2	Ukodishaji wa canteen	PA/128/2022/2023/H Q/NC/10	STAFF CANTEEN
3	Ukodishaji wa chumba cha 'stationery'	PA/128/2022/2023/H Q/NC/11	4A – BLUE HOUSE
4	Ukodishaji wa chumba cha 'stationery'	PA/128/2022/2023/H Q/NC/12	4B – BLUE HOUSE
5	Ukodishaji wa chumba cha 'stationery'	PA/128/2022/2023/H Q/NC/13	4C - BLUE HOUSE
6	Ukodishaji wa chumba cha 'stationery'	PA/128/2022/2023/H Q/NC/14	4D- MKWAWA
7	Ukodishaji wa chumba cha 'stationery'	PA/128/2022/2023/H Q/NC/15	4E – STUDENT CAFTERIA

4. Muombaji atatakiwa kuomba zabuni moja tu kati ya saba(7) zilizoainishwa kwenye jedali hapo juu
5. Waombaji waoneshe kiasi ambacho watakuwa tayari kulipa kwa mwezi kwa zabuni husika na malipo yatakuwa kwa awamu nne (miezi mitatu mitatu) kwa mwaka.
6. Upangaji wa vyumba hivi vya biashara ni wa kupindi cha kuanzia Julai mosi, 2022 hadi juni 30, 2023

7. Mpangaji wa Chumba cha Biashara atakayefanikiwa kupata chumba hataruhusiwa kumpangishia mtu mwingine (Sublets) bali kufanya Biashara yeye mwenyewe.
8. Zabuni zinatolewa kwa utaratibu wa ushindanishi, Kwa hiyo iko wazi kwa waombaji wote wenye sifa kuomba kupanga katika maeneo yaliyoainishwa.
9. Waombaji wote wenye nia na uwezo wanaweza kupata taarifa kamili kupitia makabrasha ya zabuni katika ofisi ya **OFISI YA KITENGO CHA UNUNUZI NA UGAVI - TAASISI YA MAENDELEO YA JAMII TENGERU**, kila siku kuanzia saa 2.30 asubuhi hadi saa 9:30 mchana, siku za Jumatatu hadi Ijumaa [kuondoa siku za sikukuu zinazotambulika kitaifa]
10. Nyaraka za aina zote za Zabuni zitapatikana baada ya kulipa ada ya Maombi ya Tshs 50,000/= (Hamsini Elfu). Malipo ya maombi ya zabuni yatafanyika kupitia 'control number' utakayopewa na Taasisi kupitia ofisi ya uhasibu iliyopo Jengo la Utawala. Namba za simu kwa ajili ya kupata namba ya malipo 'Control Number' ni 0756 386829. Malipo yaliyotolewa kama ada ya maombi ya zabuni hayatarejeshwa.
11. Zabuni zote zifungwe ndani ya bahasha iliyofungwa kwa lakiri [seal], na juu ya bahasha iandikwe maandishi yanayotaja Aina ya zabuni, namba ya zabuni, jengo na ziwasilishwe katika **OFISI YA KITENGO CHA UNUNUZI NA UGAVI – TICD**, kabla ya tarehe 17/06/2022 saa tano (5.00 asubuhi) kwa kutumia Anuani ifuatayo: -  
  
MKUU WA TAASISI,  
TAASISI YA MAENDELEO YA JAMII TENGERU  
S.L.P 1006  
TENGERU- ARUSHA.
12. Waombaji wote wenye sifa na uwezo wanaweza kuja kutembelea na kuona Majengo/vyumba (site visit) siku ya jumanne tarehe 14/06/2022 kuanzia saa 10:00 asubuhi mpaka saa 9:00 mchana, kukutana katika jengo la Utawala- idara ya Fedha.
13. Ufunguzi wa Zabuni hizo utafanyika mbele ya wazabuni waombaji au mwakilishi mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha Zabuni tarehe 17/06/2022 saa 5.00 asubuhi.
14. Taasisi ya Maendeleo ya Jamii hailazimiki kukubali/ kutokukubali kutoa zabuni kwa mwombaji zabuni yeyote kutokana na kigezo cha malipo makubwa/malipo kidogo ya eneo la ukusanyaji mapato au utoaji huduma linaloombewa zabuni.



**MKUU WA TAASISI  
TAASISI YA MAENDELEO YA JAMII TENGERU  
ARUSHA**